# ST. JOSEPH

## Husband of Mary Novena



**CATHOLIC ARCHDIOCESE OF MOMBASA**

# CATHOLIC MEN ASSOCIATION

***NOVENA YA MT. YOSEFU.***

## SIKU YA KWANZA.

**(LUKA 2: 1-7)**

**BABA MLEZI WA YESU.**

Mt. Yosefu ulibahatika kushiriki fumbo la utukufu kama Baba mlezi wa Yesu. Maria ndiye pekee alihusika moja kwa moja kwa ukamilifu wa fumbo hili ambapo alijitolea kikamilifu kutunga ubinadamu wa Yesu katika damu yake. Ulipata nafasi kwenye fumbo hili kwa njia pekee, kwa kukamilisha hali hii mhimu ya utungaji, utunzaji wa ubikira wa Maria kabla na hata wakati wa maisha yake ya ndoa. Ulifanya ubikira wa maisha ya ndoa kuwezekana, na hii ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu uonekane, ikubalike na itukuzwe kutoka mioyo yote. Kwa njia moja kwa moja ulishiriki kutunza, kulea na kulinda mtoto mtukufu – Yesu Kristu – Kama Baba wa Mbinguni alikutuza moyo shujaa wa ubaba, moyo uliojaa mapendo na kujitolea.

Kwa kazi ya mikono yako ulikubaliwa kumpa ulinzi mwana mtukufu kumpatia chakula, mavazi na malazi – wewe kweli umtakatifu wa utoto Mtakatifu wa Yesu – Maumbile ya uhai wa maisha yake yaliyomtunza mtoto Yesu Kristu.

Wakati Herode alipomtafuta mtoto Yesu amuue, Baba wa Mbinguni alimtuma malaika kama mjumbe na kukuletea ujumbe wa kuhama na yote akakuachia mikononi mwako. Ni upendo huu wa ubaba ambao ulikuwa ukimbizi pekee ambao ulimpokea na kumtunza mtoto huyu mtukufu. Upendo wako wa ubaba, ulimhamisha kupitia jangwani mpaka Misri hadi maadui wote walipoangamizwa.
Baadaye katika mikono yako mtoto alirudi Nazareti kulelewa na kutunzwa miaka hiyo mingi kwa kazi ya mikono yako.
Chochote mwana wa binadamu alihitaji kutoka kwa Baba, binadamu kwa faida ya kukua na kusaidika pia Yesu alihitaji kutoka kwako kwa vile kwako ulikuwa Baba mlezi, mwalimu na mlinzi wake.

Ulimtumikia mtoto huyu kwa utukufu na upendo mmoja. Mungu alikujalia moyo uliojaa upendo mkuu wa mbingu – Upendo wa ndani na wa nguvu kushinda ule wa baba yeyote mwanadamu awezao kuwa nao. Ulimtumikia mwana Mtukufu bila choyo wala kutarajia faida yoyote bali kwa kujitolea. Hukufanya kazi mwenyewe bali kwa kujitolea ulionekana kama chombo kilichotarajiwa kwa faida ya wengine. Chombo cha kuegeshwa kando mara tu kimalizapo kazi yake, kwa kutosikika tena mara tu (ujana) wa Yesu ulipopita.

Ulikuwa kivuli cha Baba wa Mbinguni sio tu kama baba wa kidunia, mwakilishi wa mamlaka ya Baba, bali pia kwa uwezo wa ubaba wako, ambao ulionekana wa kawaida ulikuwa ni uufiche kwa kiasi ule utukufu wa Yesu – mtiririko wa ajabu wa mwito wako mtukufu – mtoto mpendwa uliyembeba mikononi mwako na kumpenda na kumtunza kwa uaminifu akiwa na Mungu Mbinguni kama Baba na Mwana – Yeye mwenyewe. Kwako ni wadhifa maalum kati ya watakatifu wa ufalme wa Mungu, kwa shauri ulikuwa zaidi sehemu ya maisha hayo ya neno la Mungu

aliyemuumba mwanadamu. Katika nyumba yako ya Nazareti ambapo chini ya ulinzi wako wokovu wa mwanadamu ulitayarishwa.

Yale uliyokamilisha ulitufanyia sisi. Hu mwenye nguvu na jasiri tu katika ufalme wa Mungu, bali mrithi wa ukristu wote na uanadamu.
Urithi wako katika ufalme wa Mungu unazidi zaidi ufahari na heshima ya malaika wote, unahitaji heshima zetu maalum, upendo na pongezi.

**Mt Yosefu namshukuru Mungu kwa heshima aliyopatia Mungu kuwa Baba Mlezi wa mwanawe Mtukufu. Kama zawadi ya heshima yako kwa Mungu kwa bahati hii, nipatie neema ya upendo wa kujitolea kwa Yesu Kristu, Mungu wangu na Mwokozi wangu.**

**Nisaidie nimtumikie yeye kwa pendo la sadaka – wito wa kujitolea uliokuwa nao ulipokuwa ulimwenguni naye. Nijalie kwamba kupitia kuunganika na Yesu, mwanao mlezi, ninaweza kufikia kilele cha utakatifu ambao Mungu amenitayarishia na kuokoa roho yangu.**

**(Kuna sala maalum kila baada ya ombi la siku. Nakala imeambatanishwa hapa.Tafadhali mhakikishe inatumiwa siku zote tisa.)**

## ***SIKU YA PILI***

**MATHAYO 18 -24**
**(UBIKIRA WA MUME WA MARIA)**

Mt Yosefu, ninakuheshimu kama mume kweli wa Maria.Maandiko yanasema Yakobo alimzaa Yosefu mume wa Maria, na kwake, yeye akazaliwa Yesu aitwaye Kristo (Mathayo 1:16). Ndoa yako kwa Maria ni muunganiko mtukufu ambapo wewe na Maria mlijitolea pamoja. Maria alikuwa wako kweli vile alivyo na alivyokuwa navyo.

Ulikuwa na haki kwa pendo lake na unyenyekevu; na hakukuwepo mwengine aliyezidi pendo, sifa, unyenyekevu wa Imani ya pendo hilo. Pia ulikuwa mlinzi wa Maria. Kulingana na ndoa yenu mlijitolea ubikira wenu, pia usafi na usawa wa ubikira wenu pia ni mpango mtukufu wa kuzaliwa kwa Yesu Kristo, Kwa vile Mungu alimtuma malaika wake kukuhakikishia kwamba umama na ubikira wa Maria unaweza kuunganishwa.

Umoja huu wa ndoa sio kwamba uliwaeleza kwenye uhusiano wa kila siku wa familia na Maria pendo kuu la viumbe vya Mungu lakini pia kukuwezesha kushirikishana matunda ya kiroho. Na Maria akapata kutambulika kwake kwa unyenyekevu na utulivu, na heshima kuu, usafi na utakaso. Ni heshima kuu upatayo kutoka kwa umoja huu wa karibu naye, ambapo kwake Mwana wa Mungu humwita Mama na pia kumdhihirisha kama Malkia wa mbingu na Dunia! Vyovyote Maria alikuwa na haki ya uhusiano wako pia hii inajumuisha mwanawe, hata hivyo Maria alimpata Mwana huyu kutoka kwa Mungu kwa njia ya kiajabu. Yesu alikuhusu kama baba njia ambayo Mungu alichagua ulimwenguni, fumbo kuu, tukufu ambapo faida na baraka tele zimetufukia.

Mungu mwana alikuwa na imani kwa ulezi na usaidizi wa mamake Maria mkingiwa dhambi ya asili kwa ulinzi wako. Maisha ya Maria yalikuwa yale ya Mama wa Mwokozi, ambaye hakuja ulimwenguni kufurahia heshima na raha lakini kuokoa ulimwengu kwa kazi ngumu, mateso, na pia msalaba. Umekuwa mshiriki mwaminifu, msaidizi na mtulizi wa mama wa mwana mtukufu Jinsi gani ulivyokuwa mwaminifu kwake kwa umaskini, safarini, kazi na maumivu. Pendo lako kwa Maria lilijengwa juu ya kujitolea kwako kwa Maria kama mama wa Mungu.

Mbele ya Mungu na mwanawe mtukufu, hukumpenda yeyote zaidi kuliko Maria. Maria alijibu pendo hili. Alijitolea kwa ulezi wako kwa moyo wa kweli na neema kama mtoto mwaminifu. Roho Mtakatifu mwenyewe ndiye muunganishi wa pendo hili kuu ambao unaunganisha mioyo yenu.

**Mt. Yosefu; ninamshukuru Mungu kwa zawadi ya wewe kuwa Bikira Mume wa Maria. Kama zawadi ya heshima yako kwa Mungu, nijalie neema ya kumpenda Yesu kwa moyo wangu wote. Kama ulivyotenda na kumpenda Maria kwa unyenyekevu na uaminifu.**

## SIKU YA TATU

## ( MWANZO 41: 33 – 43)

## MWANAMUME ALIYECHAGULIWA NA KUBARIKIWA KWA UTATU MTAKATIFU

Mt. Yosefu, wewe u mwanamume uliyechaguliwa na Mungu Baba. Alikuchagua uwe mwakilishi wake hapa Duniani. Hivyo akakupatia neema zote na Baraka ulizo hitaji ili kuwa mwakilishiwe wa thamani.

Ulikuwa mume aliyechaguliwa na Mungu kuwa Baba mlezi mwenye thamani – Akakuo ngezea utajiri wake na zawadi tele juu ya yote akakupa upendo wake. Kipimo cha kweli cha utakatifu wako unashuhudiwa ni kule kujitolea kwako kwa Yesu. Ulikuwa kweli umetakatifuzwa na Yesu kufanya kazi karibu naye wakati wote.

Kumpa umuhimu wako, mateso yako, maisha yako mwenyewe, Yesu aliishi nawe kikamilifu ili uweze kujiingiza kwake. Hii inadhihirisha utukufu maalum na lengo kuu la utakatifu wako.

Hivyo baada ya Maria wewe ndiwe Mtakatifu sana kati ya watakatifu wote. Roho mtakatifu alikuchagua uwe pendo la kweli la Baba na la Mwana – na Moyo wa utukufu wa Utatu Mtakatifu katika hekima yake, Mungu anaelekeza viumbe vyote kutoka utupu hadi kikomo cha mafanikio yao na kuwaonyesha thamani yao na kuwapa uwezo wa kuifikia. Kila mwito na kila ukamilifu wa mwito hutoka kwa Roho Mtakatifu. Kama Baba Mlezi wa Yesu na kichwa cha familia ulipata kuwa mfano mzuri wa mwito – kufungua njia ya wokovu wa dunia na kutayarisha kwa kuelimisha na kumwongoza mwana wa Mungu – Mtu.

Kwa kazi hii, ulishiriki kama chombo cha Roho Mtakatifu – Roho Mtakatifu huyu ndiye kiongozi uliyemheshimu na kutenda kazi yake – Jinsi gani ulitekeleza kazi kwa heshima – ukiongozwa na Mungu wa upendo!

Maandiko ya Agano la kale ambalo Pharaoh aliyazungumza kuhusu Yosefu wa Misri yanaweza pia kuhusishwa nawe – Tunawezaje kumpata mtu mwengine ambaye amejaa Roho wa Mungu au mtu wa hekima kama yeye (Mwanzo 4:38) labda kwenye ushirika wako na kazi tukufu ya Mungu kushinda ile ya Misri – Sasa unatawala pamoja na mwanao mlezi na kuonekana kwenye kioo cha hekima ya utukufu wa Mungu na matunda ya Roho zetu.

**Mt. Yosefu; Ninamshukuru Mungu kwa kukufanya mtu maalumu aliyekuchagua kama zawadi ya hekima yako kwa Mungu – Nijalie neema ya kufuata mwenendo wako ili pia nami niweze kuufurahisha moyo wa Mungu.**

**Nisaidie nijitolee kikamilifu kwa huduma zake na ukamilifu wa mpango wa Roho wake mtakatifu ambapo siku moja niweze kufika mbinguni na niunganike kiroho na Mungu kama ulivyo.**

## ***SIKU YA NNE***

### (MATHAYO 2: 13 – 14, 19 – 21)

### MTUMISHI MWAMINIFU

Mt.Yosefu uliishi kwa lengo moja – uwe mtumishi wa karibu wa Yesu Kristu Neno aliyefanyika mwili. Umashuhuri wa kuzaliwa kwako na ukoo wako, neema na tuzo, ulizomiminiwa na Mungu, hizi zote zilikuwa juu yako kwa kumtumikia Bwana yetu vyema. Kila wazo, neno na kitendo chako, ilikuwa sifa na matokeo ya pendo na utukufu wako wa Neno Tukufu.

Ulikamilisha kiaminifu wajibu wa mtumishi mwema na mwaminifu ambaye alilinda nyumba ya Mungu.

Jinsi gani utiifu wako ulivyokamilika! Nafasi yako kwenye familia takatifu ilikubidi kuamrisha, lakini kando na kuwa Baba mlezi wa Yesu, ulikuwa pia mjumbe wake Yesu – kwa karibu miaka thelathini ulimtunza mwana wa Mungu kumuonyesha unyenyekevu na utiifu wa juu na ukaishi kupenda na kuutimiza kikamilifu wewe mwenyewe, bila kutarajia, ulijitolea kwa Mungu, utawala wa dunia, na kwa sauti utu wako.

Wakati Mungu alimtuma malaika wake kukuarifu umlinde Maria, uliheshimu licha ya fumbo lililohusu umama wake kwa Yesu.

Ulipoambiwa ukimbilie Misri wakati wa hali ngumu, ulitii bila kusema neno lolote dogo la ulalamishi – Wakati Mungu alikushauri ndotoni kurudi Nazareti, ulitii. Kwenye hali yoyote, utiifu wako ulikuwa rahisi kama imani yako, unyenyekevu kama moyo wako, na kamilifu kama pende lako – utiifu wako haukujali chochote: ulifuata kila agizo.

Ulikuwa na sifa ya kujitolea kikamilifu, na ari ya mtumishi mwema. Kila wakati wa maisha yako yalihusisha kumtumikia Bwana wetu: kulala, mapumziko, kazi, taabu, uaminifu kwa wajibu wako ulitolea kila kitu bila choyo hata furaha yake, ungetoa sadaka hata ile furaha ya kuishi na Maria. Yote hayo na mengi ya Nazereti ilikuwa sadaka ya mwito wa huduma yako.

Maisha yako yote yalikuwa ya kujitolea kwa moyo hata kufikia kiwango cha kuwa tayari kufa ili kuonyesha upendo wako kuonekana. Kwa Yesu na Maria. Kwa kujitolea kikamilifu, ulihudumu bila ya kupata sifa au zawadi yoyote.

Lakini Mungu alitaka ufahamu kwamba uko na uhusiano wa wokovu wa ulimwengu. Aliaminisha kwamba umlishi na mlezi wa Mwana Mtukufu. Alikutaka uwe maskini na kutaabika kwa sababu ya Mungu – Alikuteua kuwa Baba mlezi wa mwanawe

aliyekuja ulimwenguni kuwaokoa wanadamu kwa mateso na kifo na uwe mshiriki wa mateso yake.

Katika haya majukumu yote muhimu, Baba mwenyezi wa mbinguni alikutambua kama mtumishi mwaminifu

**Mt. Yosefu, ninamshukuru Mungu kwa bahati yako ya kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu. Kama shukrani ya heshima binafsi kwa Mungu, nijalie nami ile neema ya kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu kama ulivyokuwa. Nisaidie kushiriki kama ulivyofanya, ule utiifu mkamilifu wa Yesu aliyekuja sio kwa kuyafanya mapenzi yake – ila Mapenzi ya Babake; kutumainia mapenzi ya Mungu, nikifahamu kwamba nikifanya mapenzi yake, Atanijalia mahitaji yangu yote ya kiroho na kimwili niwe mvumilivu katika majaribu yangu na kuyaachia yote kwa Bwana wetu ili aniweke huru kwa yote wakati utakapompendeza kufanya hivyo – pia nisaidie niige moyo wako mnyenyekevu kwa kuwa haitakuwa thawabu kuu hapa ulimwenguni kuliko ile furaha na heshima ya kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu**.

## ***SIKU YA TANO***

**WAEFESO 5: 21 – 33**

**MLEZI WA KANISA**

Mt.Yosefu, Mungu amekuteua kama mlezi wa Kanisa Katoliki kwa vile ulikuwa kichwa cha familia Takatifu, chanzo cha Kanisa. Ulikuwa Baba, Mlinzi na mtunzaji na mlezi wa familia Takatifu – Kwa shauri hilo una uhusiano kwa njia mwafaka kwenye kanisa ambayo ndiyo iliyo sababu ya kupatikana kwa familia Takatifu.

Ninaamini kwamba Kanisa ni familia ya Mungu hapa ulimwenguni – Serikali yake ina wakilishwa kwa uwezo wa kipapa zaidi ya yote katika nguvu halali ya Mwili wa Kristu ambaye kweli yuko katika sakramenti Takatifu ya Altare, hivyo kuendeleza maisha ya Kristu kwenye kanisa – kutokana na nguvu hii, pia huja mamlaka juu ya Fumbo la mwili wa Kristu, Jamii ya Kanisa – Uwezo wa kuelimisha na kuongeza roho na kuzipatanisha na Mungu na kuziombea.

Una uhusiano maalumu kwenye maisha ya Kipadri kwa vile uliongoza nguvu ya ajabu juu ya Mkombozi wetu Mwenyewe. Maisha na wadhifa wako ulikuwa wa shughuli ya kipapa na hasa ikiunganika na sakramenti Takatifu. Zaidi ya yote ulikuwa chanzo cha ujio wa Mwokozi kwetu kama ilivyo kazi za Kipadri kutuletea Mwokozi kwenye Misa kwa vile ulimlea Yesu – ukamtunza – ukamkuza, ukamlinda na mabaya na hata kumpatia makao.
Ulitambulika kama Yosefu wa Misri aliyewapa watu wake ngano. Lakini sasa ajulikanaje zaidi kukuliko! Yosefu wa Kasri la zamani, Wamisiri walipokula mikate kwa uhai wao.

Ulimlea na kwa uangalifu ukatunza ukahifadhi kanisa lake ambaye ni mkate wa Mbingu na kupeana maisha ya kiroho kwenye sakramenti.
Mungu amekuteua kuwa mlezi wa kanisa kwa sababu wadhifa wa kiakida ulikufikia kwa njia maalumu. Maakida walikuwa viongozi wa familia za watu waliochaguliwa, na maisha yao yalikuwa heshima kutayarisha ujio wa Mwakozi. Yosefu wewe ulikuwa kati ya mtiririko huu wa kifalme kwa vile ulikuwa mmoja wa wale viongozi wa mwisho wa familia ya Daudi u mmoja wa wazee wa karibu wa Kristu kwa hali ya kimwili.

Kama mume wa Maria, yule mama wa Mungu, na kama baba Mlezi wa Mwokozi . Unahusika moja kwa moja na Kristu – mwito wako unaunganiko maalumu na umtu wa Yesu; shughuli zako zote zilimhusisha Yesu hivyo basi umwisho wa Agano la kale na chanzo cha Agano Jipya ambalo ni chimbuko la familia Takalifu ya Nazareti, kwa vile Agano jipya ni mwendelezo wa Agano la kale kwa heshima yote. Akida wa maakida anayeheshimika zaidi kutukuzwa na kudhaminiwa kati ya maakida wote.

Kupitia Maria kanisa lilimpokea Kristu na hivyo kanisa lina ahadi zake. Hata kanisa linatarajiwa kukurudishia heshima na sifa kwako pia, kwa vile wewe ndiwe uliyechaguliwa kumwezesha Kristu kuja ulimwenguni kulingana na sheria kwako ambapo wafalme na manabii na waumini walipokea tunda la ahadi ya Mungu. Kati ya wote hao, wewe pekee ndiye uliyeshuhudia kwa macho yako na kuwakili ahadi ya wokofu kwa watu wote

**Mt. Yosefu, ninamshukuru Mungu kwa bahati yako ya kuwa mwakilishi wa kanisa kama shukrani ya heshima kwa Mungu, nipatie neema ya kila wakati kuishi kama mtu wa maana kwa kanisa ambapo kupitia hivyo niweze kuokoa Roho yangu. Wabariki mapadri, watawa na walei wa kanisa katoliki ili waweze kuishi upendo wa Mungu na uaminifu wanapomtumikia Mungu – Likinge kanisa kutoka maovu yote ya siku zetu na mateso kutoka kwa maadui wake. Kupitia uwezo wako na uhusiano wako – naliombea kanisa kukamilisha kisawa lengo lake hapa ulimwenguni la utukufu wa Mungu na Wokovu wa roho zetu.**

## *SIKU YA SITA*

### LUKA 2: 51,YOSHUA BIN SIRA 30: 1 - 6

#### MLINZI WA FAMILIA

Mt Yosefu ninakuheshimu kama kiongozi mnyenyekevu wa familia Takatifu – Familia Takatifu ndiyo jukwaa la kazi ya maisha yake, tangu mwanzo wake – ulezi wake na ulinzi wake kupitia wajibu wako kwa Kristo na Maria na hata kufikia kifo chake mwenyewe katika mikono yao. Uliishi, ukatembea na kutenda katika upendo wa muungano wa Yesu na Maria.

Waandishi waliofunuliwa na Roho wa Mungu wataja maisha yake ya Nazareti kwa maelezo machache tu. "Na Yesu aliambatana nao na kwenda Nazareti na kuwa mtoto wao: Luka 2:51
Basi Yesu akarudi pamoja nao hadi Nazareti akawa anawatii na mama yake akaweka mambo hayo yote moyoni mwake"

"Naye Yesu akaendelea kukua katika hekima na kimo akazidi kupendwa na Mungu na watu". Ambapo maneno haya yanaeleza kule kujitolea zaidi kwa mwito wako hapa ulimwenguni na mtiririko wa neema iliojaza Roho yako wakati wa siku zile ulizoishi Nazareti.

Maisha yako ya familia huko Nazareti yaliangaza utukufu wa huruma – kulikuwa na ushirikiano wa kuigwa kwa washiriki wote wa familia yake Takatifu. Hakungekuwa na muungano wa karibu kama ule wa wakukuunganisha na Yesu, Mwanao mlezi na kwa Maria, Bibi yako mpendwa.

Yesu alichagua kukutimizia wewe Babake Mlezi, majukumu yote ya Mwana mwaminifu, kukupatia ishara ya heshima imstahiliyo mzazi. Na Maria akakuonyesha kila ishara ya heshima na upendo wa Bibi aliyejitolea, uliitikia upendo huu kwa heshima kutoka Yesu na Maria kwa hisia za upendo na heshima ya ndani kwa vile Yesu alikuwa na upendo kamili wa ubaba, heshima na moyo dhati kwa Roho Mtakatifu. Na hungeweza kufurahia kazi za neema za Moyo wa Maria na, kuvutia huku kulifanya lile pendo tukufu ulilompatia Maria siku ile ya harusi yenu kuwa na nguvu zaidi siku zote.

Mungu amekuteua kuwa mlezi wa familia kwa sababu ulijinyenyekeza kuwa kichwa na kiongozi wa Familia Takatifu na kuwa shauri ya mfano wa sifa zako nzuri unatukuza maisha ya ndoa. Ni amani na furaha iliyoje kwa Familia Takatifu kuwa chini ya ulinzi na sheria za ubaba wako, hata kwenye majaribio.

Ulikuwa mlinzi, mshauri na mwamuzi wa Familia Takatifu kwenye mahitaji yote. Na vile ulikuwa mfano wa uchaji wa Mungu! Ulitupatia mfano mzuri wenye ari na mfano wa kumtumainia Mungu kuthibitika hasa zaidi kwa pendo lako kwenye mfano wa wajibu wako kulingana na mapenzi ya Mungu. Ulipitia wajibu wote

ambao ni muhimu kwa maisha ya familia kudibithi utukufu wa maisha, mateso, na furaha kwenye muungano wenu na Yesu na Maria – Kwa hivyo familia ni muhimu kwako kama kazi ya Mungu, na ni ya kipeo cha juu katika macho yako ili kukufanikisha hazina ya Mungu na ufanisi wa mwanadamu katika upendo wa kibaba na mafanikio wewe ndiwe mlezi na kiunganishi cha familia, na unahitaji heshima na nafasi kwenye familia zote.

**Mt. Yosefu – ninamshukuru Mungu kwa bahati yako ya kuishi kwenye familia Takatifu na pia kuwa kichwa chake; kama zawadi ya heshima yako kwa Mungu ;ipatie familia yangu Baraka za Mungu – Fanya nyumba yangu kuwa makao ya kifalme ya Yesu na Maria – makao ya kifalme yenye amani, furaha na upendo.**

**Ninaziombea familia zote za kikristu kwamba tunahitaji msaada wako wakati wa siku hizi ambako maadui wa Mungu huzisumbua na kuzivunja. Mbele ya macho haya maovu, kama mlezi wa familia, uwe na ari ya kusaidia kwa hiari kama vile zamani ulivyosimama na kumwokoa mtoto Yesu na mamaye, pia leo simama na ulinde utukufu wa nyumba zetu. Fanya nyumba zetu ziwe nyumba Tukufu za sala, upendo – na sadaka za moyo na huduma . Ziwe mifano bora ya Nazareti. Kaa nasi pamoja na Yesu na Maria, ili kwa msaada wako, tuweze kuheshimu amri za Mungu na za kanisa; kupokea sakramenti Takatifu za Mungu na za Kanisa; Tuishi maisha ya sala; kufuata mafundisho ya dini katika nyumba zetu.**
**Tujalie hayo ili tuunganike kwenye ufalme wa Mungu wa maisha ya kiroho tukiunganika na familia Takatifu Mbinguni.**

# *SIKU YA SABA*

## MLEZI WA WAFANYIKAZI

## MT 5:3 – 12, WATHESOLONIKE (2) 3:6 – 14

Mt.Yosefu ulijitolea muda wako Nazareti kufanya kazi ya useremala. Ilikuwa nia ya Mungu kwamba wewe na mwanao wa kulea mtumie siku zenu pamoja katika kazi ya sulubu. Jinsi gani ulivyowekea mfano mzuri kwa wanaofanya kazi! Ilikuwa hasa kwa maskini, ambao ndio wengi wa idadi ya watu ambao Yesu alijia ulimwenguni kwa vile katika sinagogi la Nazereti alisoma maneno ya Isaya na kujitaja mwenyewe.

Roho wa Bwana yu juu yangu kwa maana ameniteua kuleta 4:18. Ilikuwa nia ya Mungu kwamba ufanya kazi inahusishwa na maskini, yaani kwamba kwa njia hii, Yesu mwenyewe aitweze kwa kurithi kutoka kwako, babake mlezi na kihiari aikubali. Hivyo basi, Bwana wetu anatufundisha kuwa, kwa wale wa daraja la wafanyakazi wanyenyekevu, ametuwekea neema zake tele ilmradi waishi katika kutosheka pale Mungu alipowatuma na kubaki maskini wa Roho kwa maana amesema.” Heri walio maskini wa Roho maana ufalme wa mbinguni ni wao. (Mat 5:3)

Ile kazi uliyojitolea kwayo katika karakana huko Nazereti. Ilikupa fursa nyingi ya kujizoesha unyenyekevu. Ulibahatika kuona kila siku mfano wa unyenyekevu ambao Yesu alifanya thawabu inayompendeza mno. Alichagua kwa makazi yake sio makasri ya wana wa waflme wala mafua kumbi za wasomi, lakini karakana ya Nazereti. Hapa ulijishirikisha kwa miaka mingi unyenyekevu na uficho wa utenda kazi wa Mungu – mwanadamu. Jinsi gani ilivyo mfano wa kielelezo kwa mfanyikazi wa kileo.

Huku mikono yako ikishughulika na kazi ya sulubu, akili yake ilielekezwa kwa Mungu katika sala. Kutoka kwa Bwana mtakatifu alifanya kazi pamwe nawe, ulijifunza, kufanya kazi na Mungu katika ile Roho ya sala kwa kuwa alifanya kazi na kumcha Babake na kupendekeza ushirika wa ulimwengu kwa Kristu, Yesu pia alikuagiza katika neema za ukweli na thawabu kwa kuwa ulikuwa daima karibu nawe aliyejisemea.” Ndimi njia ya ukweli na uzima.

Ulipokuwa ukifanya kazi katika taaluma yako, ulikumbushwa ukuu na uweza wa Mungu, ambaye kama mchora ramani za ujenzi hodari aliunda mbingu yote kwa ujuzi wake maridhawa na nguvu zake. Mwangaza wa amani uliojaza akili yako haukufifia ulipoona yesu akifanya kazi kama seremala. Uliamini kabisa kuwa yule kijana mtakatifu aliyefanya kazi bega kwa bega awe alikuwa kweli mwana hasa wa Mungu.

**Mt. Yosefu, namshukuru Mungu kwa bahati yako ya kuweza kufanya kazi bega kwa bega na Yesu katika karakana yako ya Nazareti. Kama zawadi ya shukrani zako kwa Mungu, nipatie neema ya kuheshimu kazi na kutosheka na nafasi yangu maishani, hata kama ni ya chini ambayo nimewekwa. Nifunze kumfanyia kazi Mungu katika hali ya unyenyekevu na sala kama ulivyofanya, ili niweze kutoa utokaji jasho wangu katika kuungana na kujitolea kwa Yesu katika Misa kama msamaha wa dhambi zangu na kupata ustahiki mkuu mbinguni.**

## ***SIKU YA NANE***

**(LUKA 2: 27 – 35)**

**RAFIKI KATIKA MATESO**

Mt. Yosefu sehemu yako ya mateso ilikuwa kubwa sana kwa sababu ya ukaribu wako na Mwokozi. Maisha yake yote yalikuwa tu mateso na zaidi ya mateso. Umaskini ulikukalia na msalaba wa kazi ukakuandama kila mahali. Na misalaba ya kinyumbani kutokana na kuishi na mtakatifu na aliyeheshimiwa kati ya binadamu wote, Yesu na Maria ambao wote walikuwa kwako. Hasa ilikuwa yale mateso yaliyosababishwa na kutokuweko uhakika wa ubikra wa Maria kwa kule kuwekewa jina la Yesu ambayo ilielekeza mikosi ya baadaye. Uchungu tena wa kina lazima ulileta na ule utabiri wa Simioni, safari ya Misri, kupotea kwa Yesu hekaluni wakati wa kusherehekea Pasaka. Mateso yote haya yalikuwa uongezo wa huzuni ya ndani machoni pa dhambi za watu wako mwenyewe.

Ulibeba mateso haya yote katika njia ya ukweli kama Yesu na katika hili wewe umfano wetu. Hakukua na manung'uniko wala sauti za usio subira zilizokutoka ---- hakika ulikuwa Mtakatifu mkimya! Ulikubali yote katika Roho wa imani, unyenyekevu, uhakika na upendo. Kwa furaha ulipokea yote kwa ajili ya Mwokozi na Mama yake, ukijua kwamba pendo la kweli ni pendo la kusulubiwa. Lakini Mungu hakukuacha katika majaribu yako. Na majaribu pia yalipotea na yakabadilishwa mwishowe kuwa faraja na furaha.

Inaonekana kama Mungu alikuwa amenuia maisha yako yajazwe na mateso na pia faraja ili kuleta mbele yangu ukweli kuwa maisha yangu duniani ni mpito wa furaha na huzuni na kwamba ni lazima nikubali kwa shukrani chochote Mungu anachonitumia na wakati wa faraja nijitayarishe kwa mateso. Nifunze kubeba msalaba wangu katika roho ya imani, uhakika na shukrani kwa Mungu. Katika furaha ya milele, nitamshukuru Mungu mno kwa mateso aliyonitumia wakati wa hiji yangu duniani ambayo baada ya mfano wako nilivumilia na kuingiwa na upendo kwa Yesu na Maria.

Hakika ulikuwa shahidi wa imani wa maishafishe. Hii ilikuwa nia ya Mungu, kuwa yule mtu awaye mwongofu, ndiye zaidi hujaribiwa kwa ajili ya upendo na utukufu wa Mungu. Ikiwa kuteseka ndiko kuchanuka maua kwa neema za Mungu katika roho na ushindi wa roho kwa upendo wa Mungu, kuwa Mtakatifu mkuu baada ya Maria, basi uliteseka zaidi ya shahidi yeyote wa imani.

Kwa sababu umeshuhudia mateso ya bonde hili la machozi, umwingi wa huruma na imani kwa wale walio na uhitaji. Katika vizazi hata vizazi roho, zimekugeukia wewe katika shida na kukupata ukiwa rafiki mwaminifu katika mateso. Umesikia sala zao

hata ingawa zilihitaji miujiza. Kwa kuwa uliunganika karibu sana na Yesu na Maria maishani mwako, kutuombea kwako na wao ni kwa nguvu zaidi.

**Mt. Yosefu, namshukuru Mungu kwa bahati ya kuweza kuteseka kwa ajili ya Yesu na Maria. Kama zawadi ya shukrani zako kwa Mungu , nipatie nami neema ya kukubali mateso yangu kisubira kwa ajili ya Yesu na Maria. Nijalie kuunganisha mateso, kazi mavunjiko moyo ya maisha na kujitolea kwa Yesu katika Misa na kushiriki kama wewe katika roho ya kujitolea ya Maria.**

## *SIKU Y A TISA.*

**(YOHANA 17: 1 -5, 11 -12)**
**MLEZI WA KIFO CHA FURAHA**

Mt Yosefu, jinsi gani ilivyopendeza kuwa katika wasaa wako wa kufa, Yesu asimame kando ya kitanda chako na Maria, utamu na tumaini la ulimwengu. Ulijitolea maisha yako yote kwa ajili ya huduma ya Yesu na Maria, kwa kifo ulifurahia faraja ya kufa mikononi mwao mwa upendo. Ulikubali kifo katika kupenda kupokea nia ya Mungu na kukubali huku kulifikisha kileleni maisha yakofiche ya wema. Yako ilikuwa hukumu ya huruma, kwa mwanao mlezi ambaye ulikuwa umemtunza kwa upendo, alikuwa hakimu wako na Maria wakili wako. Uamuzi wa hakimu ulikuwa neno la kuhimizwa kusubiri kuja kwake ambako angekumiminia matunda chaguo kukombolewa na ukumbatio wa shukrani ya upendo kabla kupumulia mwanao roho wa milele.

Ulitazama kuliko milele na zawadi ya milele na uhakika. Ikiwa Mwokozi wetu alibariki wachungaji, Mamajusi, Simoni, Yohane M'batizaji na wengine kwa sababu walisalimu uwepo wake kwa mioyo ya kujitoa kwa saa moja lakupita, je kwa kiasi gani tena zaidi anaweza kuwa alikubariki uliyejitakasa kwa miaka mingi ukiwa naye na mama yake? Ikiwa Yesu anachukulia kila matendo ya huruma na kazi ya huruma, zilizofanywa kwa niaba ya wanaume wenzetu kwa upendo wake, kama alivyofanyiwa na kuahidi mbinguni kama zawadi, nini ambacho lazima kilikuwa shukrani yake kwako katika ukweli wa neno kwamba wewe ndiye uliyempokea, ukampa malazi, mavazi, ukamlisha na ukamfariji kwa kujitolea nguvu zako na mapumziko na hata maisha yako kwa pendo lililopita la kina baba wote.

Mungu kweli na kibinafsi alijifanya mdeni kwako. Mwokozi wetu alilipa deni hilo la shukrani kwa kukupa neema nyingi maishani mwako, hasa neema ya kukua katika pendo ambalo ndio zawadi nzuri na safi kati ya zawadi zote. Hivyo mwisho wa maisha yako moyo wako ulijazwa mapendo ambayo mwili wako mnyonge wa kutamani hangeweza kuzuia. Roho yako ikafuata ushindi wa upendo wako na kuruka duniani kupokea manabii na mashahidi katika furaha ya ujio wa Mwokozi

**Mt. Yosefu, nakushukuru kwa bahati yako ya kuweza kufa mikononi mwa Yesu na Maria. Kama zawadi ya shukrani zako kwa Mungu, nipatie neema za kifo cha furaha. Nisaidie kutumia kila siku yangu katika maandalizi ya kifo. Na pia, nikubali kifo katika hali ya kujiachilia katika mapenzi ya Mungu na kufa kama ulivyofanya, mikononi mwa Yesu kupata nguvu za Viaticum na mikononi mwa Maria, na rozari mkononi mwangu na jina lake kinywani mwangu!**

# **NOVENA KWA MT. YOSEFU**.

## **( Sala isemwe mwisho wa ombi la kila siku)**

Mt. Yosefu, Mimi mwanao nisiyestahili, nakusalimu. Wewe ni mlinzi mwaminifu na mwombezi wa wote wanaokupenda na kukuinua. Unajua nina uhakika maalum kwako na baada ya Yesu na Maria, ninaweka tumaini langu la uokovu kwako kwa maana una nguvu na Mungu na hutawaacha watumishi wako waamini. Hivyobasi, ninakunyenyekea na kujileta mwenyewe pamoja na wote waliowapendwa wangu na vyote vilivyo vyangu, kwa maombezi yako.

Nakuomba kwa pendo lako kwa Yesu na Maria, usiniache wakati wa maisha na unisaidie katika saa ya kufa kwangu.
Mt. Yosefu, mchumba wa Bikra mteuliwa, nipatie akili safi, nyenyekevu na karimu na kujisalimisha kamili kwa mapenzi yake Mungu. Kuwa mwongozo wangu na kielelezo changu katika maisha ili nistahili kufa kama ulivyofanya mikononi mwa Yesu na Maria. Mpenda Mt. Yosefu, mfuasi kamili wa Yesu Kristu, nakuinulia moyo wangu kuitisha maombezi yako ya nguvu ili kupata Moyo wa Yesu neema zote za mambo yangu ya kiroho na uendelezo wa kimaisha, hasa neema ya kifo cha furaha na neema maalumu ninayoomba:

( **Taja ombi lako ……………)**

Mlinzi wa neno teule, nina hakika kwamba sala zako kwa niaba yangu zitasikika mbele ya ufalme wa Mungu. Amina

**KUMBUKA**.

**Kumbuka ee Bikira Maria mpole sana, haijasikika kamwe kwamba ulimwacha mtu aliyekimbilia ulinzi wako, aliyeomba msaada na maombezi yako.**
**Kwa matumaini hayo, nakukimbilia, ee Mama, mkuu wa mabikira. Ninakuja kwako, nasimama mbele yako, nikilalamika mimi mkosefu, ewe Mama wa neno la Mungu. Naomba usikatae maneno yangu, bali uyasikilize. Amina.**

Tunajua Yosefu alikuwa mtu wa imani, mtiifu kwa lolote Mungu alilomwomba afanye pasi kujua litakalotokea. Malaika alipomjia Yosefu katika ndoto na kumwambia ukweli kuhusu mtoto ambaye *Maria alikuwa amembeba, Yosefu mara moja na bila maswali wala uhitaji wa masengenyo, alimchukuwa Maria kama mkewe. Malaika alipokuja tena kumwambia familia yake ilikuwa hatarini, mara moja aliwacha kila kitu alichokuwa nacho, yeye na familia na rafiki zake wakaenda nchi geni na mkewe mchanga na mtoto. Alisubiri Misri bila udadisi wa maswali mpaka malaika alipomwambia ilikuwa salama kurudi.*